# MEDICAL LABORATORY SCIENTISTS' ASSOCIATION OF TANZANIA (MeLSAT)

**P.O. Box 65094**
**Dar es Salaam.**

**Email: president@melsat.or.tz**
**Tel: +255 222 128 052**
**+255 784 756 340**
**www.melsat.or.tz**

**Ofisi ya Rais MeLSAT**

## TAARIFA KWA WANACHAMA

Ndugu wanachana wa MeLSAT, awali ya yote nawasalimu wa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kama viongozi wenu kwanza tunaishukuru Serikali yetu pendwa kwa kuwa inatambua mchango wa Wataalamu wa Maabara nchini kote na mara zote imekuwa ikitupatia ushirikiano wa kutosha pindi tunapowaomba kukutana nao na kujadili yale yote yanayohusu taaluma ya Maabara.

Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wanachama wote nchini kufuatia kadhia mbalimbali zilizojitokeza siku za hivi karibuni kuhusiana na taaluma yetu hapa nchini, aidha napenda pia kuwafahamisha kuwa chama kinaendelea kufuatilia maslahi ya wanachama walio ndani ya ajira na wale ambao bado hawajapata fursa ya kuajiriwa. kama mnavofahamu wiki chache zilizopita ilitoka taarifa ya Muundo pendekezwa kwa Kada zilizo chini ya Wizara ya Afya, ambapo upande wetu baadhi ya mapendekezo yalikuwa hayajaakisi kile tulichokipendekeza wakati wa tuliposhiriki majumuisho ya muundo huo.

Katika kufuatilia maslahi ya walio ndani ya ajira, Chama kilipokea hoja kutoka maeneo mbalimbali na tulichukua hatua stahiki, ambapo tuliomba kukutana na viongozi wa idara husika, tulikubaliwa. Wajumbe wa chama wakiongozwa na Makamu wa Rais wa MeLSAT waliweza kufika jijini Dodoma kufanya kikao siku ya tarehe 3 na 4 Juni, 2025. Kufuatia kikao hicho kilichohusu Muundo chama kilikuwa katika hatua za mwisiho za kukamilisha taarifa ya kikao hicho na itatolewa kwenu kupitia Ofisi ya Katibu Mtendaji wa MeLSAT.

Aidha, mpaka sasa tumefanikiwa kupata miadi ya Kwenda Dodoma na kuonana na watendaji wa Ofisi ya sekretarieti ya Ajira, ambapo siku ya leo tarehe, 19 Juni, 2025 watakaa na viongozi ili kuweza kuzifikisha hoja za msingi juu ya uchache wa nafasi za ajira kwa upande wa wataalamu wa Maabara za Afya.

Hatua nyingine zilizochukuliwa na Chama zinaendelea kufanyiwa kazi na viongozi wa Kanda kupitia kwa viongozi wa mikoa. Hivyo basi naomba nitoe wito kwa Waratibu kote nchini kutoa ushirikiano pindi utakapoombwa ushirikiano kutoka kwa kiongozi wa MeLSAT katika Mkoa wako.

Mwisho, wakati tunalishughulikia suala hili, niwaombe tena ndugu wanachama wa MeLSAT nchini kote, tuendelee kuwa watulivu na wenye subira huku tukiendelea kufanya kazi ya kuwatumikia watanzania wenzetu. Taarifa ya mchakato wote itatolewa ikishakamilika.

*Umoja wetu ndiyo nguvu yetu.*

Ahsante

Medical Laboratory Scientists Association of Tanzania * MeLSAT *

**Yahya R. Mnung`a**

Rais – MeLSAT

**19.06.2025**